Jina: ______________________________ Tarehe: ______________

Nambari ya mwanafunzi(**KNEC ASSESSMENT NO.**) ______________________

Gredi ______________________ Jinsia: Mvulana ☐ Msichana ☐

Jina la shule ______________ Nambari ya Shule ☐☐☐☐

**KWA MATUMIZI YA MTAHINI**

**Mwalimu ajaze mjalizo baada ya kusahihisha kazi ya mwanafunzi**

**Viwango vya kutathmini**

| **ZOEZI** | **Kuzidisha matarajio** 4 | **Kufikia matarajio** 3 | **Kukaribia matarajio** 2 | **Mbali na matarajio** 1 |
|---|---|---|---|---|
| Kusoma kwa sauti 10 | Ana uwezo wa kusoma kwa kasi bila kusita. Anazingatia alama zote za uakifisho. | Ana uwezo wa kusoma bila kusita. Anazingatia baadhi ya alama za uakifisho. | Ana uwezo wa kusoma, isipokuwa anasitasita. Hazingatii alama za uakifisho. | Hana uwezo wa kusoma maneno mengi. Hazingatii alama za uakifisho. |
| Kusikiliza na kuzungumza **(alama 5)** | **5** | **4** | **2 - 3** | **0 - 1** |
| Sarufi/Ufahamu/ kuandika **(alama 35)** | **35** | **30 - 34** | **11 - 29** | **0 - 10** |

## SEHEMU YA A: ZOEZI (i)

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

**Sikiliza hadithi ya mwalimu kisha ujibu maswali.**

Bwana Kibara ni mkulima hodari. Yeye huishi katika kijiji cha Mitinane. Katika shamba lake, amefuga sungura, kondoo na kuku wa mayai. Pia amepanda mahindi. Kazi hii ya ukulima imemsaidia sana. Ameweza kujenga nyumba ya kifahari. Mwaka uliopita, alivuna mahindi magunia arubaini na moja. Alipoyauza mahindi yake, alipata pesa alizozitumia kulipia mtoto wake karo ya shule. Bwana Kibara ana wafanyakazi wanane katika shamba lake.

**a)** Bwana Kibara hufanya kazi gani? **(Mwanafunzi ajibu)**
**b)** Taja wanyama anaowafuga Bwana Kibara. **(Mwanafunzi ajibu)**
**c)** Kazi hii ya ukulima imemsaidia aje? **(Mwanafunzi ajibu)**
**d)** Mwaka jana alivuna mahindi magunia mangapi? **(Mwanafunzi ajibu)**
**e)** Pesa alizozipata baada ya kuuza mahindi alizifanyia nini? **(Mwanafunzi ajibu)**

## KUSOMA KWA SAUTI

**Soma kifungu hiki kwa sauti.**



Siku moja, watoto walipanga sherehe ya siku ya uzalendo. Walivalia mavazi ya rangi za bendera na walifanya maonyesho ya sanaa na michezo. Wakati wa sherehe, walipanda miti kama ishara ya kutunza mazingira. Watoto walifurahia sana na walijivunia kuwa raia wa nchi yao.

## SEHEMU YA B

## UFAHAMU ZOEZI (ii)

**Soma hadithi kisha ujibu maswali**



Jumamosi iliyopita, shangazi yangu alitutembelea. Hakuwa ametutembelea kwa muda wa wiki mbili. Aliniletea peremende na biskuti. Baba na mama walifurahi sana kumwona. Hata hivyo, nilikuwa na furaha kuliko wao. Siku iliyofuata, Jumapili, mimi na shangazi tuliienda kanisani ambapo tuliimba na kumchezea Mungu. Ilikuwa ni siku njema.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

1. Shangazi wa mwandishi aliwatembelea siku ya ____________________
2. Shangazi wa mwandishi alimletea nini? ____________________
3. Mwandishi alienda kanisani siku ya ____________________
4. Akina mwandishi ____________________ kumwona shangazi. **(walikasirika, walifurahi)**
5. Walipokuwa kanisani, walifanya nini? ____________________

## SARUFI

**Andika majina ya picha hizi**

6. 

____________________

7. 


____________________

8. 

____________________

9. 

____________________

10. 

____________________

**Tumia "Yeye" au "Wao" kujaza nafasi**

11. ____________ wanalima shamba.
12. ____________ ataenda sokoni.
13. ____________ watafuata sheria.
14. ____________ anacheza vizuri.
15. ____________ watanawa mikono yao.

**Onyesha silabi katika maneno haya**

**Mfano: raha - ra + ha**

16. Mwizi = ____________________
17. Mwanafunzi = ____________________
18. Mwinuko = ____________________

**Andika sentensi zifuatazo kwa wingi**

19. Mwalimu amekuja darasani.

____________________



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

20. Kiti kimevunjika.

______________________________

21. Mimi ni mtoto mzuri.

______________________________

22. Mvulana amelala.

______________________________

**Tunga sentensi ukitumia maneno yafuatayo.**

23. Hasara ______________________

24. Sokoni ______________________

**Tumia "-ako" au "-enu" kujaza pengo.**

25. Mapera ______________

26. Kikapu ______________

27. Viberiti ______________

**Kanusha vitendo hivi**

28. Cheka ______________________

29. Soma ______________________

30. Ruka ______________________

## KUANDIKA

**Andika sentensi tano kuhusu:-**

**LIKIZO YA APRILI**

31. ______________________________

32. ______________________________

33. ______________________________

34. ______________________________

35. ______________________________



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com